**MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA**

*Karatasi ya maswali: namba 6*

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa 'Kazi ya ziada' unaweza kulijibu swali kama ukipenda, au kuliacha kama unaona huliwezi. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

**MASOMO: 21- 23**

20 A. Nakili na ukikamilishe kifungu hiki (utahitaji maneno zaidi ya moja kwa baadhi ya majibu).

Roho Mtakatifu ni ………………. wa Mungu. Mungu ……………………….. mbingu na nchi kwa kutumia ……………… yake. Maneno ya kwenye Biblia ni maneno yake. Aliitumia …………………. yake kuwaambia walioandika nini waandike, kwa hiyo Biblia inaelezewa kuwa ni 'Neno lenye ……………………. ya Mungu'.

Yesu alizaliwa kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Ni uweza wa Mungu uliomfanya …………………….. ashike mimba ya Yesu, na Yesu alipewa huo uweza, ambao ni Roho ya Mungu, wakati ……………………………….. Aliutumia uweza huo ……………………………………………………………………

Roho Mtakatifu anaitwa pia 'Mfariji' au 'Msaidizi'. Ni uweza uliotolewa kuwasaidia ………………………… kwa njia ya kuwakumbusha mambo Yesu aliyowaambia. Tunasoma juu ya nguvu hiyo akiwashukia wanafunzi wa Yesu katika Matendo, Sura ya ………… Baada ya Bwana Yesu…………………………………………. nguvu hiyo iliondolewa.

B. Zawadi (au karama) za Roho Mtakatifu zilitolewa kwa ajili gani?

C. Zilitolewa zidumu kwa muda gani?

21.A. Kati yake zilizokuwa za maana zaidi ni zipi?

B. Ni zawadi ( au karama) ipi iliyo ya muhimu kuliko zote? (1Wakor. 13)

C. Ni watu gani waliokuwa na uwezo wa kuwapa watu wengine zawadi (au karama ) hizo?

D. Je! Zipo hata leo?

22. A. Biblia inatuambiaje juu ya jinsi Adamu alivyoumbwa?

B. Hawa aliumbwaje?

C. Ni nyoka aliyewafanya Adamu na Hawa wale tunda la mti uliokatazwa?

D. Adhabu ya Adamu kwa kumkiuka Mungu ilikuwa ni nini?

E. Ni kwa nini watu wote wanakufa?